# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO**

**SHULE YA SEKONDARI LUSANGA**

**P.O. Box 150**
**Lusanga –Turiani**
**Morogoro – Tanzania**

**Mkuu wa shule: +255 787738944** **E-mail lusangasec1990@gmail.com**
**Matron +255 719672919**
**Patron +255 756361306**
**Malezi. +255 719889912**

**Tarehe: 29/ 04/ 2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**

**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LUSANGA HALMASHAURI YA MVOMERO MKOA MOROGORO MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya HGL/ HGK/ CBG / PCB.

Shule ya Sekondari LUSANGA ipo umbali wa Kilometa 115 kutoka Mjini Morogoro. Unaweza kufika mji mdogo wa **Madizin**i ukitokea Morogoro Mjini Kituo cha Mabasi **Msamvu** au Dares Salaam (Magufuli Bus Stand). Ukiwa Kituo cha Mabasi cha Magufuli cha Dar es Salaam uliza Mabasi ya kwenda Turiani (*KVC, HOPE Safari au BM COACH)* na ukiwa Morogoro uliza NOAH, COASTER au BASI za kwenda **Turiani**,.Mabasi haya yatakufikisha hadi Mji mdogo wa Madizini kituo cha Mabasi ambapo utapata usafiri wa kuja shuleni ambao ni pikipiki kwa gharama ya Tsh: **1,500**/= na 5,000/= (kwa Tax). Mwendo wa kutoka Kituo cha Mabasi cha Magufuli Dar es Salaam hadi Mji mdogo wa Madizini ni Masaa saba (7). Na mwendo kutoka Morogoro mjini (kituo cha mabasi Msamvu) hadi mji mdogo wa Madizini ni masaa mawili (2).

Kwa wale wanaotokea Dodoma kuna gari la moja kwa moja liitwalo *HC Safari*, kutoka Dodoma hadi mji mdogo wa **Madizini** kituo cha Mabasi ambapo utapata usafiri wa kuja shuleni ambao ni pikipiki kwa gharama ya Tsh: **1,500**/= na 5,000/= (kwa Tax).

Kwa wanaotokea njia ya Arusha/Moshi/Korogwe/Handeni, kuna magari ya moja kwa moja ambayo ni *Mipango ya Mungu*, *KVC Safari* na *Mapenzi ya Mungu*, mwambie dereva akushushe kituo kiitwacho "**Kwa Temu**" (shule ya msingi Lusanga) simama kama unaangalia gari linakoelekea, mkono wako wa kulia utaiona barabara ya vumbi hatua kama 25 utaliona geti la Shule ya Sekondari Lusanga.

Kwa wanaotokea njia ya TANGA/Korogwe/Handeni, kuna gari la moja kwa moja ambalo ni *SIMBA MTOTO*, mwambie dereva akushushe kituo kiitwacho "**Kwa Temu**" (shule ya msingi Lusanga) simama kama unaangalia gari linakoelekea, mkono wako wa kulia utaiona barabara ya vumbi hatua kama 25 utaliona geti la Shule ya Sekondari Lusanga.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **01/07/2024**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **29/06/2024** Siku ya Jumamosi kuanzia saa **2:00 asubuhi** hadi saa **12:00 jioni.** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/07/2024.**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi 2 (mbili) kitambaa rangi ya kijani esteem namba 01 mshono wa rinda box (ziwe ndefu zifike kifundo cha mguu),(*zinapatikana shuleni*)

ii. Mashati mawili meupe mikono mifupi (wasiovaa hijabu na mikono mirefu kwa wanaovaa hijabu),(*zinapatikana shuleni)*

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni **nyeupe isiyo na urembo (kitambaa cha halua)** ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

iv. Sare ya Michezo ni Track suit 2 (mbili) rangi ya light blue (bluu bahari),*(zinapatikana shuleni)*

v. Viatu vya shule ni jozi mbili vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

vii. Sweta mbili rangi ya kijani, (*zinapatikana shuleni*).

viii. Nguo za kushindia sketi 02 mbili rangi ya dark bluu mshono wa rinda box (ziwe ndefu zifike kifundo cha mguu), *(zinapatikana shuleni)*
ix. Tai 02 (mbili) rangi ya kijani yenye mistari ya rangi nyeupe
x. Tisheti (T-shirt) mbili rangi ya kijivu (zinapatikana shuleni)
xi. Tisheti (T-shirt) Maalumu ya Shule, *(zinapatikana shuleni)*

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 7 kwa wanafunzi wanaosoma Tahasusi ya Sanaa na Madaftari 11 kwa wanafunzi wanaosoma Tahasusi za Sayansi
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology.
v. Scientific Calculator.
vi. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe vipimo vya futi 2.5 au 3.
vii. Mashuka Jozi 2 light blue na pinki, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 nyeupe (pembe nne)
viii. Nguo za ndani za kutosha.
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe) visiwe vya Plastiki.
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Vifaa vya usafi kulingana na mchepuo

| MCHEPUO | AINA YA VIFAA |
|---|---|
| HGL | Slesha + ndoo ya lita 20 +Dawa ya kusafishia vyoo/tiles (ARO LITA 1) |
| HGK | Slesha + ndoo ya lita 20 + Dawa ya kusafishia vyoo/tiles (ARO LITA 1) |
| CBG | Squizer + cobweb remover +Dawa ya kusafishia vyoo/tiles(NEW TRILIONNAIRE PURE CLEANER LITA 1) |
| PCB | Jembe/mpini +soft broom + Dawa ya kusafishia vyoo/tiles (NEW TRILIONNAIRE PURE CLEANER LITA 1) |

**ANGALIZO:**

**VIFAA VYA USAFI, SARE ZOTE ZA SHULE NA MAHITAJI MENGINE PIA YANAPATIKANA SHULENI KWA GHARAMA NAFUU KWA ATAKAYEHITAJI**.

### 2.2 MAHITAJI YAFUATAYO YANAPATIKANA SHULENI

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Nembo | 5,000/= |
| 2. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **10,000/=** |

### 2.3 MICHANGO MBALIMBALI

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| | **Jumla** | **70,000/=** |

**MUHIMU: Michango yote ya jedwali 2.3 iwekwe kwenye Akaunti ya shule 22001200012- NMB. Fedha taslimu (cash) haipokelewi.**
**Jina: LUSANGA SEKONDARI.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:-

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- ❖ **Mwanafunzi anapaswa kuja na kadi ya BIMA YA AFYA kwa ajii ya matibabu awapo shuleni, hivyo mzazi unapaswa umkatie mwanao bima kabla ya kuripoti shuleni (NI LAZIMA).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu, na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.\
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA LUSANGA**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule: BAHATI M. OMARY**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ……………………………** MKUU WA SHULE SHULE SEKONDARI LUSANGA S. L. P. 150, TURIANI

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule + 255 787 738 944**
- **Makamu Mkuu wa Shule + 255 715 524 058**
- **Mwandamizi Taaluma + 255 712 408 806**
- **Mwandamizi Malezi +255 753 124 996 / +255 715 459 404**

**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI LUSANGA**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**

picha

**A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

- JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………
- TAREHE YA KUZALIWA……………………………………………..……
- MAHALI ALIPOZALIWA (MKOA/ WILAYA) …………………………………
- MAHALI ANAPOISHI (KATA/MTAA) ........................................................
- URAIA ……………………………………………………………………….
- SHULE ALIYOTOKA………………………………………………………….
- NAMBA YA MTIHANI/USAJILI………………………………………………..

**B: TAARIFA YA MZAZI:**

- JINA LA MZAZI/MLEZI

  ……………………………………………………………………………………

- KAZI YA MZAZI/MLEZI ……………………………………………………
- ANUANI YA MZAZI/MLEZI …………………………………………………..

- SIMU YA MZAZI/MLEZI (tafadhali andika namba zinazotumika na mhusika kama ni mama au baba

  n.k) ………………………………………………………………………………………

**C: KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA (MWANAFUNZI)**

Mimi …………………………………………. Kidato ……mwaka……… Nimesoma na kuyaelewa yote. Kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo au maelekezo bila kulazimishwa kuyazingatia.

Tarehe ………………………. Sahihi ……………………

D: **KUKUBALI SHERIA ZA SHULE :( MWANAFUNZI)**

Mimi ………………………………… nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na naahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu na viongozi wote wa shule, nikikiuka sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe …………………… Sahihi ……………………….

**E: MZAZI/MLEZI – (Ajaze sehemu hii)**

(i) Mimi Mzazi/Mlezi wake nathibitisha kuwa Mwanangu (jina la mtoto)………….…………………………… ameelewa maagizo na ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanangu ni………………………… dhehebu lake ni …………………………….

(ii) Ninaruhusu/Siruhusu (kata isiyohusika) mwanangu kushiriki katika Makongamano au Warsha za kidini nje ya shule zinazofanyika nje ya Mkoa wa Morogoro pasipo na Mwalimu wa shule hii.

(iii) Ninaruhusu/Siruhusu (kata isiyohusika) wakati wa likizo fupi (mid-term) atoke shuleni na kwenda kwa…………………………wa (mahali)………………… Uhusiano wake na Mwanangu ni …………………………Namba yake ya simu ni ………………………

(iv) Ninaruhusu wafuatao wamtembelee mwanangu siku maalum ya kuona wanafunzi

(1) …………………………… (anakoishi)…………… (simu)……….............

(2) …………………… ………. (anakoishi)……………..…. (Simu)………..………

(3) …………………………..... (anakoishi)…………………..(simu)………………...

***MUHIMU***: **kutembelea mwanafunzi ni mara mbili kwa muhula**, tofauti na hapo **hutopokelewa**.

Pia mwanao ataruhusiwa kwenda likizo fupi kwa mtu au mahali ulipoelekeza wewe hatutapokea mabadiliko kulingana na maelekezo ya mwanafunzi.

(v) Aidha mimi ……………………………………….…….. ambaye ni Mzazi/Mlezi,

nimesoma/nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi (jina la mwanafunzi)……………………………na kuahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

| ***……………..………*** | ***………………..…….*** | ***……….………………..*** |
|---|---|---|
| ***JINA LA MZAZI/MLEZI*** | ***SAHIHI YA MZAZI / MLEZI*** | ***TAREHE*** |

**F. SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU**

Ndugu wa karibu wanaoruhusiwa kumtembelea mtoto:

BABA MAMA

| JINA | UHUSIANO |
|---|---|
| 1.......................................................... | ......................................... |
| 2......................................................... | ......................................... |
| 3............................................................ | ......................................... |
| 4........................................................... | ......................................... |

5.......................................................... ..........................................

MLEZI -01 MLEZI-02 MLEZI-03

**G. KIKAO CHA WAZAZI**

Kitafanyika mara moja kwa mwaka wa masomo 2024/2025.Wazazi/walezi mtapewa taarifa siku na tarehe ya kikao hicho.

**Masharti mahususi**:

1. Ni lazima mzazi/mlezi kuhudhuria kikao
2. Udhuru wowote hautakubalika
3. Kwa mzazi/mlezi asiyefika siku ya kikao atalipa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000) Vinginevyo mwanafunzi hatapokelewa na atalazimika kurudi alikotoka

**H. SEHEMU YA MZAZI KUKIRI KUHUDHURIA KIKAO CHA WAZAZI**

Mimi..................................................mzazi wa ......................................wa kidato cha .................... Nitahudhuria kikao cha wazazi bila kukosa hapo shuleni kwa tarehe itakayopangwa

............................................... ................................ ..........................

Jina Sahihi Tarehe

KARIBU SANA LUSANGA SEKONDARI

.....................................................

MKUU WA SHULE
SHULE SEKONDARI LUSANGA
S.L.P. 150, TURIANI

Bahati M. Omary.
MKUU WA SHULE

**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A**

**From: The Headmistress**
Lusanga Secondary School,
P.O. Box 150,
**Turiani - Morogoro**

**To**
**The Medical officer,**
**………………………………………**
…………………………………………
…………………………………………… (Name of student in full) Please examine the named above student as to her physical and mental fitness for a full time student. The examination should include the following categories (a-d)

(a) (i) Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Venereal disease (v) Limbs
(vi) Leprosy (vii) Epilepsy
(b) Neurosis
(c) Other serious diseases eg. Asthma, Tb etc
(d) **Pregnancy**

Name: BAHATI M. OMARY Date: 12TH JUNE 2023

MKUU WA SHULE
SHULE SEKONDARI LUSANGA
S. L. P. 150, TURIANI

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)
I have examined the above student and consider that she is fit/unfit for full time studies.

(i) Eyesight………………………………………….
(ii) Hearing…………………………………………
(iii) Speech …………………………………………
(iv) Limbs…………………………………………..
(v) Venereal diseases………………………………
(vi) Leprosy ……………………… (vii) Epilepsy ………………………………………….
(viii) Neurosis……………………
(ix) Other serious e.g. Asthma …………… T.B…………
(x) Pregnancy ……………………

**Other Comment**

**…………………………………………………………………………………………………………………………………………………**

**Name ………………………………………….. Date ………………. Signature …………….**

**STATION …………………………… DESIGNATION** …………………………………

**LIST OF BOOKS.**

1. ENGLISH LANGUAGE/LITERATURE
    - AN INTODUCTION TO LINGUISTIC, LANGUAGE GRAMMA & SEMANTICS (2007) BY JINDAL. D.
    - AN INTRODUCTION TO LANGUAGE (2007).BY FROMKIN. V
    - ADVANCED ENGLISH LANGUAGE 5&6 (2001) BY JOHN, J. OXFORD
    - ADVANCED LEVEL ENGLISH.A PRACTICAL APPROACH (2010) BY NICHOROUS, ASHERI.
    - ADVANCED LEARNER'S DICTIONARY (**COMPULSORY**)
    - **NOVELS:**
      A MAN OF THE PEOPLE
      BEAUTIFUL ONES ARE NOT YET BORN
      HIS EXCELLENCY HEAD OF STATE
      SEASON OF WAITING
    - **PLAY:**
      AN ENEMY OF THE PEOPLE
      BLACK MAMBA
      BETRAYAL IN THE CITY
      I WILL MARRY WHEN I WANT
    - **POETRY**
      ENCOUNTER FROM AFRICA
      SELECTED POEMS FROM EAST AFRICA

    } AT LEAST 2 BOOKS IN EACH CATEGORY

2. KISWAHILI SARUFI/FASIHI
    - NADHARIA YA LUGHA, KISWAHILI 1 KIDATO CHA 5&6 (2016). J.A MASEBO & NYANGWINE
    - NADHARIA YA FASIHI, KISWAHILI 2 KIDATO CHA 5&6 (2016). J.A. MASEBO & NYANGWINE.
    - SAMIKISA (SARUFI MIUNDO) MASAMBA NA WENZAKE

- SAMAKISA (SARUFI MAUMBO)
- VUTA NI KUVUTE (SHAFII A. SHAFII)
- KAMUSI

3. HISTORY
    - AFRICA FROM NEOLITHIC REVOLUTION TO PRESENT (ZISTI KAMILI) 2012
    - CONTEMPORARY HISTORICAL EVENTS ADVANCED LEVEL HISTORY ONE (COMRADE SHIBITAL C.K. TUMAINI)
    - HOW EUROPE UNDERDEVELOPED AFRICA (WALTER RODNEY 2001)
    - MASTERING MODERN WORLD HISTORY (HAMPSHIRE PALGAVE. (NORMAL LOWE 1997)
    - THE MODERN WORLD SINCE 1870, (LONGMAN GOUP LTD, HONGKONG)
    - A HISTORY OF AFRICA VOL.1 (ASSA OKOTH 1915-1995)
    - NOMAN LOWE (20130 MASTERING MODERN WORLD HISTORY
    - PEACOEK (1982) 7TH EDITION: THE HISTORY OF MODERN EUROPE FROM 1789 – 1981.

4. GEOGRAPHY
    - DAVID WAUGH & NELSON THORNES (2009/ANY), GEOGRAPHY AN INTERGRATED APPROACH, 4TH EDITION, PRINTING INTERNATIONAL LTD.
    - COLIN BUCKLE (1978) LANDFORMS IN AFRICA, AN INTRODUCTION TO GEOGRAPHY, LONGMAN GROUP LTD
    - JOHN M. PRITCHARD (1984), PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA.LONGMAN GROUP LTD.
    - R.B. BURNET (1988), PHYSICAL GEOGRAPHY IN DIAGRAMS FOR AFRICA. LONGMAN GROUP LTD HONGKONG.
    - COTHARI (2013), RESEARCH METHODOLOGY.
    - GOH CHENG LEONG & GILLIAN C. MORGAN (1973), HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY, 2ND EDITION, OXFORD UNIVERSITY PRESS.
    - KIBUUKA P. KARUGGAR & MUGO M. (20050.CERTIFICATE GEOGRAPHY FORM 4. OXFORD UNIVERSITY PRESS.

5. BASIC APPLIED MATHEMATICS
    - BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS (TIE)

- BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED LEVEL BY RESPICIUZI KIIZA & LUGANO MWANGINDE.
- BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS BY SEPTINE INYASI SILLEM.
- BASIC APPLIED MATHEMATICS REVIEW BOOK FOR PROBLEMS AND SOLUTIONS 1998 – 2013 BY IMMACULATA MOSHA & YAHYA KAWIA.

6. BIOLOGY
    - BIOLOGICAL SCIENCE (BS)
    - BIOLOGY FUNCTIONAL APPROACH
    - UNDERSTANDING OF BIOLOGY

7. CHEMISTRY
    - MODERN'S ABC OF CHEMISTRY CLASS XI – PAT I & II.DR.S.P. JAUHAR
    - ADVANCED LEVEL PHYSICAL CHEMISTRY WITH GENERAL CHEMISTRY (APE NETWORK). MARK DANIEL & HERMES DARMIANS.
    - CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASS XI.S. CHAND
    - GENERAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK. FIVE & SIX. (TIE)
    - PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK. FORM FIVE & SIX (TIE)
    - ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK. FORM FIVE & SIX. (TIE)
    - INORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK.FORM FIVE & SIX.

8. PHYSICS
    - A-LEVEL PHYSICS BY ROGER MUNCASTER 4$^{TH}$ EDITION
    - NEW UNDERSTANDING PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL 4$^{TH}$ EDITION
    - PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL BY TIE
    - CHAND'S PRINCIPLE OF PHYSICS FOR CLASS XI OR XII
    - SCIENTIFIC CALCULATOR (**COMPULSORY**) AVAILABLE AT SCHOOL.

9. GENERAL STUDIES
    - KAMILI ZISTI (2017). GENERAL STUDIES ALIVE.A STRAIT FORWARD GENERAL & DEVELOPMENT STUDIES FOR HIGH SCHOOLS & UNIVERSITY STUDIES.DAR ES SALAAM KAMILI BOOKS & GENERAL SUPPLIES. (THE BEST BOOK)

- BIGIRWAMUNGU J & DEOGRATIAS S (2018). UNDERSTANDING GENERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL.DAR ES SALAAM. AFRICA PROPER EDUCATION NETWORK.